

TAARIFA KWA UMMA

1. Utangulizi

PSPTB ni taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 23 ya mwaka, 2007, pamoja na majukumu mengine PSPTB huendesha mafunzo na mitihani ya kitaaluma. Ili kutekeleza matakwa ya Sheria PSPTB iliendesha mitihani ya kati awamu ya Pili ya Taaluma ya mnyororo wa Ugavi nchini kuanzia tarehe 30.08 – 04.09.2026.

2. Udahili na Matokeo ya mitihani ya Kati Awamu ya Pili ya PSPTB

(a) Udahili

Mitihani hii ilidahili jumla ya watahiniwa 567

(b) Waliofanya mitihani

Jumla ya watahiniwa 528 walifanya mitihani huku watahiniwa 39 wakikosa mitihani husika kwa sababu mbalimbali.

(c) Ufaulu kwa ujumla

Watahiniwa 275(52.1%) wamefaulu kati ya watahiniwa 528 na watahiniwa 232(43.9%) wanarudia masomo yao na watahiniwa 21(4.1%) wamefeli na wataanza upya masomo yao katika ngazi husika.

3. Pongezi

PSPTB inatoa pongezi

- (a) Watahiniwa waliofaulu mitihani yao katika ngazo zote.
- (b) Watahiniwa waliopata sifa za kutunikiwa Vyeti vya Professional Diploma, Graduate Professional na CPSP.
- (c) Wahadhiri na Wakufunzi kutoka katika vyuo na vituo vya mafunzo kwa kuwasaidia watahiniwa kuweza kufanya vyema

4. Mwaliko wa kushiriki Mahafali ya 15 ya PSPTB kwa wale waliofaulu Professional Diploma (I&II), Graduate Professional (I,II&III) na Research.

5. PSPTB inatoa Wito kwa watahiniwa wa mitihani ya PSPTB, wanafunzi wa vyuo na kwa wazazi na wadhamini kama ifuatavyo;

- (a) Watahiniwa waliofeli Mitihani hii wanawahimiza kujisaliji tena na kurudia masomo yao kwenye mitihani ya kati iliyopangwa kufanyika kuanzia **09** mpaka **13 Novemba 2026**. Dirisha la Usajili kwa ajili ya mitihani hii limefunguliwa kuanzia tarehe **08.09.2026** mpaka **24.10.2026**.

- (b) Aidha Bodi inatoa wito kwa watahiniwa wenye **referral status** ambazo ni **last chance** kuhakikisha wanatumia **VYEMA** kipindi cha Novemba 2026 kwa ajili ya kufanya mitihani na kufaulu ngazi za mitihani walizoko. Baada ya muda huo kupita **referral status** zao zitafutwa kwa mujibu wa matakwa ya mtaala wa Bodi.
- (c) Wanafunzi waliomaliza vyuo vikuu nchini au nje ya nchi wanakaribishwa kujisajili kwa ajili ya kufanya mitihani ya kitaaluma ya PSPTB ili kuwapatia sifa stahiki katika fani ya Ununuzi na Ugavi.
- (d) Wazazi na wadhamini mbalimbali wakiwemo waajiri wanapewa wito wa kuwalipia ada ya maandalizi na za mitihani watahiniwa wa mitihani hii. Hii itaongeza chachu ya wataalam katika fani hii muhimu kujiongezea maarifa na ujuzi,
- (e) Aidha Bodi inazidi kusesitiza kwamba Watahiniwa wote wa mitihani ya taaluma ya fani ya Ununuzi na Ugavi wajiepushe na vitendo vya ukiukwaji wa kanuni na taratibu za mitihani kwani Bodi haitasita kuchukua hatua kali ili kuhakikisha maadili (integrity) katika tasinia ya Ununuzi na Ugavi inaenziwa na wadau wote. Adhabu hizo kwa mujibu wa Kanuni ni pamoja na kufuata matokeo ya mitihani yote, kuwasimamisha watanihiwa mikao mitatu ya mitihani, kupewa adhabu ya kulipa fedha au kifungo jela.